# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 023 ISSN 1821 - 8253 JANUARI - FEBRUARI 2016



# Zanzibar inazidi kupiga hatua katika kutekeleza Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2011

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Said J.Ameir

**Waandishi**
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili linatolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.



P.O.Box: 2422
Zanzibar - Tanzania
Phone: +255 223 081/5
Fax: 024 223 3722
Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Kudumisha amani, utulivu na usalama ni jukumu la kila mtu

Suala la amani kwa muda mrefu limekuwa ndio agenda kuu na muhimu kwenye vikao vingi vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Aidha, viongozi wa madhehebu yote ya dini wamekuwa wakilizungumza kwa mapana suala la amani wanapokuwa ndani ya ibada zao na hata kwenye mahubiri yao mbali mbali nje ya nyumba zao za ibada.

Umuhimu wa agenda hii unatokana na unyeti wa suala lenyewe na athari kubwa inayopatikana pale ambapo amani inatoweka.

Mara kadhaa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikielezea kwa furaha na fahari kubwa kutokana na mafanikio yake ambayo imekuwa ikiyapata katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Bila ya shaka mafanikio hayo yametokana na amani na utulivu.

Katika kuadhimisha miaka 52 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alielezea mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta mbali mbali.

Licha ya kuwepo matukio kadhaa yanayoathiri kasi ya ukuaji uchumi wa dunia, uchumi wa Zanzibar uliendelea kukua na kuimarika kila mwaka. Kwa mfano, mwaka 2014 Pato halisi la taifa lilikua na kufikia asilimia 7.0.

Kadhalika, Pato la mtu binafsi nalo limeongezeka hadi kufikia TZS 1,552,000 (USD 939) mwaka 2014 ikilinganishwa na TZS 1,384,000 (USD 866) mwaka 2013 sawa na ongezeka la asilimia 12.1.

Ni dhahiri hali hiyo imechangiwa na mambo mbali mbali, lakini zaidi ni kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini kutokana na kuwepo kwa vivutio vya utalii na kuwepo kwa hali ya amani, utulivu na usalama nchini.

Kumeripotiwa mafanikio makubwa katika sekta ya kilimo na hasa kilimo cha mboga mboga kinacholimwa kwa njia ya umwagiliaji. Taarifa zinasema kuwa pato la mkulima limeongezeka sana kutoka wastani wa Tsh. Milioni 3.5 hadi shilingi milioni 5.075 kwa kila msimu.

Soko kubwa la wakulima wa mboga mboga nalo linategemea kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa biashara ya utaliii ambayo nayo inategemea hali ya amani, utulivu na usalama nchini. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikieleza wazi msimamo wake katika suala zima la kusimamia amani nchini kote.

Harakati za Serikali za kusimamia amani mara nyingi huonekana wazi wazi pale ambapo hali inakuwa mbaya kiasi ambapo imeanza kuathiri harakati za kijamii. Huu ni ule wakati ambapo vikosi vya ulinzi na usalama vinaingia mitaani huku vikiwa vimebeba silaha za moto.

Hali ya amani utulivu ambayo hailazimishi vikosi hivyo kuingia mitaani, haimaanishi kwamba vikosi vya ulinzi na usalama havifanyi kazi yake. Inawezekana kabisa kwamba hali hiyo inatokana na ama wananchi wenyewe kufahamu umuhimu wa kuwa na amani, au juhudi za vikosi hivyo za kugundua mapema dalili zinazoashiria kuvunjwa amani na kuchukua hatua zinazofaa katika wakati muafaka.

Katika hali ya kawaida, wananchi wenyewe ndio wanaopaswa kuhakikisha kuwa wanadumisha amani kabla ya kulazimisha vyombo vya dola kutekeleza jukumu lake la kusimamia amani kwa kuingia mitaani wakiwa na silaha. Ifahamike kwamba wakati nchi hasa Zanzibar ikifikia hatua hiyo, tayari biashara ya utalii itakuwa imeshapata msukosuko.

Hivyo ni vyema na ni jambo la busara kwa vyombo vya dola kuifanya kazi yao kitaalamu ili viweze kugundua mapema njama au mipango yoyote ya kuvuruga amani na utulivu ili hatua za kufaa zichukuliwe mapema kabla ya athari kubwa kuweza kutokea.

Kwa upande mwengine, wananchi nao hawana budi kufahamu athari za kuvunjika kwa amani na utulivu ili hali iliyopo iweze kuendelea. Hilo litawezekana iwapo tu kila mtu atatekeleza wajibu wake na kutoa taarifa kwa vyombo husika mara tu anapobaini dalili za kutaka kuvunjika amani, akijua kuwa matokeo ya hali hiyo humuathiri kila mmoja wetu.

# Zanzibar inazidi kupiga hatua katika kutekeleza sheria ya Mtoto ya Mwaka 2011.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na wananchi waliohudhuria hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi jengo la mahakama ya watoto lililojengwa Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja tarehe 8 Februari, 2016. Kulia ni Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Omar Othman Makungu. Kushoto ni Waziri Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Zainab Omar Mohammed*

Uanzishwaji wa mahakama za watoto ni moja kati ya hatua muhimu zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza Sheria ya Mtoto Zanzibar ya mwaka 2011, miaka mitano baada ya kuanzishwa sheria hiyo.

Mwaka 2015 wakati Zanzibar ilipotunukiwa tuzo ya dhahabu kutokana na kuwa na Sheria ya Mtoto Zanzibar yenye viwango vinavyostahiki si wananchi wengi waliotambua sababu hasa ya Zanzibar kupewa tuzo hiyo.

Lakini sasa karibu miaka 5 tangu kupitishwa sheria hiyo, Zanzibar imeshuhudia hatua mbali mbali za kisera, kiutawala na kisheria za kuimarisha mazingira mazuri yatakayowezesha ustawi wa watoto unaozingatia ulinzi na haki zao za msingi.

Sheria hiyo inaweka mazingira muafaka ya kiulinzi wa kisheria na wa haki nyingine kwa watoto wanapokuwa mbele ya vyombo vya sheria hususan mahakamani wakiwa ama watuhumiwa au mashahidi.

Kwa hivyo, uanzishwaji wa mahakama za watoto ni hatua moja muhimu na ya msingi katika kutekeleza sheria hii ili kuhakikisha haki za watoto zinalindwa.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Omar Othman Makungu wakati akiwasili katika sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi jengo la mahakama ya watoto inayojengwa Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja, tarehe 8 Februari, 2016.*

Ndio maana tangu kupitishwa kwa sheria hii zimekuwepo jitihada za makusudi zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na washirika wake kuanzisha mahakama za watoto nchini.

Kwa sasa Zanzibar ina mahakama moja tu ya watoto iliyoko Vuga ambayo ilifunguliwa rasmi mwaka 2013. Kwa hivyo kwa sasa karibu kesi zote za watoto zilizo nje ya Mkoa wa Mjini Magharibi zimekuwa zikiendeshwa katika mahakama za mikoa husika.

Ni jambo jema kueleza kuwa katika kipindi kifupi kijacho Zanzibar itakuwa na mahakama nyingine mbili na kufanya jumla ya mahakama 3 za watoto. Itakumbukwa kuwa hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliweka jiwe la msingi la mahakama ya watoto ya Mahonda katika mkoa Kaskazini Unguja. Jengo hili linatarajiwa kufunguliwa mwezi Aprili mwaka huu.

Katika hafla hiyo ilielezwa kuwa kwa upande wa Pemba, mahakama ya watoto imo mbioni kuanzishwa katika jengo la mahakama ya Chake Chake ambalo linafanyiwa ukarabati mkubwa na linatarajiwa kumalizika hivi karibuni.

Hatua hizi za haraka za kutekeleza sheria hii ya Mtoto Zanzibar ni kilelezo kingine cha dhamira ya kweli ya serikali ya Awamu ya Saba ya kutekeleza kwa vitendo Sheria ya Mtoto ili kuhakikisha ulinzi na ustawi wa watoto unapewa kipaumbele kinachostahiki.

Wahenga walisema "kuzaa mwana si kazi, kazi ni kulea" basi hatua hizi zinadhihirisha pia utayari wa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Saba katika kupanga na kutekeleza programu zake mbali mbali za maendeleo na ustawi wa jamii.

Kazi za ujenzi na uanzishwaji wa mahakama za watoto zinakwenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya Serikali ya Awamu ya Saba ya kuimarisha dhana ya utawala bora na utawala wa kisheria.



Ni ukweli ulio wazi na kuthibitishwa duniani kote kuwa watoto wanapokabiliwa na mashitaka au kutakiwa kutoa ushahidi katika mazingira ya kawaida ya mahakama mara nyingi wanashindwa kufanya hivyo.

Mbali ya kushindwa wakati mwingine mazingira hayo huwaletea athari zaidi ikiwemo za kisaikolojia na hata kukumbwa na msongo wa mawazo hivyo kuwazidishia madhila hasa kwa mtoto aliyedhalilishwa.

Kwa hivyo uanzishwaji wa mahakama za watoto ni hatua maridhawa ya kuwawezesha watoto kuwa katika mazingira bora ambayo yatawawezesha kujieleza pasi na hofu ya waliowatendea mabaya au wanaotoa ushahidi dhidi yao.

Kwa mujibu wa Jaji Mkuu Omar Othman Makungu mahakama hizo zimezingatia kanuni za uendeshaji wa mahakama za watoto kwa mfano kuweka chumba maalum ambacho mtoto atatoa ushahidi pasi na kuangaliana uso kwa uso na mtuhumiwa hivyo kuondoa kabisa hofu kwa watoto kutoa ushahidi.

Hivyo hatuna budi kukiri na kupongeza jitihada hizi kubwa zinazofanywa na Idara ya Mahakama chini ya Jaji Mkuu katika kusimamia utekelezaji wa sheria ya Mtoto na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Mapitio na Marekebisho ya Sheria (2013-2018).

Jitihada hizo kwa mujibu wa Jaji Mkuu zimeleta mafanikio makubwa katika uendeshaji wa kesi za watoto ambapo sasa humalizika haraka.

Miongoni mwa mambo yaliyosaidia kumalizika kwa haraka ni ushirikiano kati ya Idara ya Mahakama, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Chini ya ushirikiano huo kabla kesi kuanza taasisi hizo hushauriana namna ya kuweka mazingira bora ya kuendesha kesi hizo.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Said Hassan Said wakati akiwasili katika sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi jengo la mahakama ya watoto inayojengwa Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja tarehe 8 Februari, 2016.*

Aidha, kuanza kutumika kwa kanuni za uendeshaji wa kesi za watoto na kukamilika kwa taratibu za kukusanya ushahidi pamoja na mafunzo kwa mahakimu wa mikoa kushughulikia kesi za watoto kumechangia sana mafanikio haya katika eneo hilo la utoaji haki.

Mambo mengine yaliyochangia mafanikio hayo ni kuwepo kwa Kituo cha Jamii cha Kurekebisha Tabia ambacho huwapokea watoto waliopatikana na makosa na kutumikia adhabu zao.

Halikadhalika mchango wa Kituo cha Msaada wa Sheria Zanzibar ambacho kinatoa msaada wa kisheria kwa watoto wanaokabiliwa na mashtaka mahkamani.

Kwa hivyo ni dhahiri kuwa mafanikio haya ni jitihada za pamoja kati ya Serikali na washirika mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo awali hivyo hatuna budi kuwashukuru wote wanaoshirikiana na serikali katika kutimiza malengo ya sheria ya Mtoto ya Zanzibar na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Mapitio na Marekebisho ya Sheria.

Kumalizika kwa mahakama ya Mahonda na Chake Chake ambapo kutafanya idadi ya mahakama hizo Zanzibar kuwa 3 utawezesha watoto wenye matatizo ya kisheria kupata huduma mapema na kuwapa nafasi kuendelea na shughuli zao ikiwemo masomo.

Jambo la msingi ni kwa mahakama hizo kuzingatia sheria hiyo ambayo inaelekeza usikilizwaji wa kesi za watoto ufanywe haraka na kutolewa hukumu pasi na kuchelewa.

Wahenga walisema "kinga ni bora kuliko tiba".Katika mnasaba huo jarida lako linapenda kusisitiza wito alioutoa Mheshimiwa Rais wa kutaka jitihada zaidi zichukuliwe kupiga vita unyanyasaji na udhalilishaji watoto katika jamii.

Pamoja na Mheshimiwa Rais kutambua mchango wa taasisi mbalimbali katika kuielimisha jamii na kuunga mkono kampeni dhidi ya udhalilishaji na ukatili wa jinsia lakini anaitaka jamii nayo irudi katika mila na desturi ya malezi ya watoto ili kujenga taifa lenye maadili mema.

"mtoto aendelee kuwa wa jamii kama zamani ambapo malezi hayakuzingatia mtu mmoja mmoja bali jamii nzima iliwajibika"alieleza Dk. Shein na kuongeza kuwa watu wabaya wanaoharibu watoto wasipewe nafasi katika jamii na wapewe majina ya "karaha" yanayosadifu tabia zao kama ilivyokuwa zamani kwani wamepoteza heshima katika jamii.

Tunakubaliana na wito wa Mheshimiwa Rais kwa kuwa pamoja na takwimu kuonesha kesi za udhalilishaji watoto nchini zinaonesha kupungua lakini takwimu hizo lazima zichukuliwe kwa tahadhari kubwa kwa kuwa si kesi zote za aina hiyo hufikishwa katika vyombo vya sheria.

Jitihada hizi za serikali na washirika wake kuanzisha mahakama za watoto zimefungua ukurasa mpya na kuleta matumaini mapya kwa wazazi na jamii kwa jumla kuhusu ulinzi na ustawi wa watoto hapa Zanzibar.

Hata hivyo, mzigo mkubwa sasa uko kwa watendaji wa taasisi zinazohusika na utoaji haki kuanzia Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Idara ya Mahkama yenyewe na Wazazi na walezi wa watoto wamekuwa na tabia ya kuficha kesi au kutatua matatizo ya watoto kifamilia.

Kwa hivyo ni juu ya wahusika wote kuzidi kushirikiana katika kubuni mbinu bora zaidi na mikakati makini katika kushughulikia kesi za watoto kuanzia uchunguzi hadi kesi kupelekwa mahkamani na kutolewa kuhumu.

# Umuhimu wa kuharakisha Sheria ya matumizi ya mitandao Zanzibar unazidi kubainishwa



Matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanaendelea kushika kasi duniani kote na kuleta mapinduzi makubwa ya kimaendeleo katika sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na urahisi na uharaka wa kusambaza habari kwa njia tofauti.

Mabadiliko haya ya kiteknolojia ya kisasa yamewanufaisha watu wengi hapa nchini kwani wameweza pia kuitumia fursa hiyo kujifunza mambo tofauti kupitia mitandao ya kijamii kwa kupata taarifa mpya kila mara na kuelimishana kuhusu shughuli za maendeleo katika nchi tofauti na wakati huo huo wakilinganisha kasi ya maendeleo baina ya nchi yao na mataifa mengine duniani.

Kwa kutumia mitandao, wajasiriamali sasa wanaweza kufahamu hali ya soko kila siku jambo ambalo linawawezesha kufanya maamuzi ya uhakika kuhusu wapi na wakati gani waende kuuza bidhaa zao. Vile vile, imekuwa rahisi katika dunia ya leo kufahamu wapi unapata bidhaa unayoihitaji na kuweza kuinunua kupitia kwenye mitandao.

Wazazi, walezi na wanafunzi wengi wameanza kusahau kutumia muda mwingi kusimama kwenye mstari kufanya malipo ya ada za skuli kutokana na utaratibu mpya wa kisasa wa kuweza kufanya malipo hayo kwa kutumia njia za mitandao. Imekuwa ikifanyika hivyo pia katika kulipia huduma nyengine muhimu za kijamii kama vile umeme, maji, huduma za simu na malipo mengine mengi.

Lakini kwa kuwa kila maendeleo yanakuja na changamoto zake, kumekuwa ni kilio kikubwa pia juu ya matumizi mabaya ya mitandao hiyo katika jamii. Kwa mfano jamii imekuwa ikishuhudia aina mbali mbali za taarifa na picha za faragha za wanandoa zikisambazwa kwenye mitandao ya kijamii na kuleta usumbufu mkubwa wa kisaikolojia siyo tu miongoni mwa wanandoa husika lakini vile vile kwa familia za wanandoa hao.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kama zilivyo Serikali za nchi nyengine nyingi duniani, inaamini kwamba kuwepo kwa mitandao ya kijamii kunaimarisha uhuru wa wananchi wa kutoa maoni yao na hivyo kutekeleza matakwa ya kikatiba kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Ibara ya 18 kuhusu uhuru wa wananchi kutoa maoni yao.

Hata hivyo, kwa upande mwengine, SMZ inaamini pia kwamba matumizi hayo ya mitandao, yanaweza kuwa chanzo kikuu cha kuvuruga amani ya nchi, iwapo hatua za makusudi hazitochukuliwa kuharakisha matumizi ya Sheria ya mitandao ambayo pamoja na mambo mengine itatoa miongozo ya matumizi ya mitandao na kuweka adhabu kwa wale watakaokwenda kinyume na Sheria hiyo.

Umuhimu wa Sheria hiyo kwa hapa Zanzibar umezidi kuonekana katika siku za hivi karibuni ambapo baadhi ya wananchi wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii kuwakashifu watu wengine pamoja na kutoa taarifa za uongo zinazolenga kuchafua amani ya nchi ambayo imedumu kwa muda mrefu sasa.

Wapo wanaobeza umuhimu wa kuweko kwa Sheria hiyo wakijenga hoja kwamba, kuwa na Sheria ni jambo moja, lakini utekelezwaji wa Sheria yenyewe ni jambo jengine ambalo ni muhimu zaidi. Hoja hii inajengwa kutokana na ukweli kwamba Zanzibar ni moja kati ya nchi zenye Sheria nyingi nzuri ikilinganishwa na nchi nyengine duniani. Lakini vile vile Zanzibar inaongoza kwa watu kuvunja Sheria zao wenyewe bila ya kuchukuliwa hatua.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inawalinda wananchi na inawahakikishia kuwa katika utumiaji wa taarifa na utoaji wa maoni, utu wa mtu unaheshimika na hakuna aliye na haki kisheria ya kuweza kumdhalilisha mwenzake. Ibara ya 15 (1) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inaeleza kwamba "Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafasi yake, maisha yake binafsi na ya nyumbani kwake, na pia, heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake".



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akitoa hotuba yake kwa Wananchi katika sherehe za kilele cha siku ya sheria Zanzibar zilizofanyika katika viwanja vya Victoria Garden Mjini Unguja. Kushoto kwa Mhe. Rais Jaji Mkuu wa Zanzibar Omar Othman Makungu na kulia kwake ni Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Mohammed Othman Chande. Sherehe hizo zilifanyika tarehe 10 Februari, 2016*

Wakati tunazungumzia maendeleo hayo, wapo watu wachache wanaotumia fursa hiyo kuvuruga amani kwa kuchochea vurugu, kufitinisha na kuwadhalilisha watu kwa kutoa taarifa za uongo kuipotosha jamii kupitia kwenye mitandao ya kijamii bila ya kuchukuliwa hatua.

Mawasiliano kwa njia ya intaneti na mitandao ya kijamii imekuwa ikitoa changamoto kubwa kwa Tume za Uchaguzi duniani hasa wakati zinapofanyika chaguzi mbali mbali. Athari za mitandao ya kijamii katika uchaguzi zimeweza kuonekana wazi wazi katika chaguzi za hivi karibuni Tanzania Bara, Zanzibar na hata nchini Uganda, ambako Serikali iliamua kuifungia mitandao yote ya kijamii wakati wa uchaguzi.

Wigo wa matumizi ya mitandao umepanuka zaidi kwa baadhi ya watumiaji wa mitandao hiyo kufanya vitendo vya wizi (utapeli) kupitia huduma za mawasiliano na ugomvi baina ya makundi, mambo ambayo yanahatarisha usalama na hatimaye kupelekea uvunjifu wa amani ya nchi.

Aidha, ni kosa la jinai kutumia mawasiliano vibaya kama ilivyoainishwa katika Sheria ya mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) ya mwaka 2010 na kutaka mawasiliano yatumike vizuri kudumisha amani ya Tanzania.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika hotuba yake kwenye sherehe za siku ya Sheria Zanzibar hivi karibuni, alielezea kusikitishwa kwake na matumizi mabaya ya mitandao katika jamii kinyume na silka, mila na utamaduni wa Zanzibar.

Kadhalika, Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Omar Othman Makungu kwenye maadhimisho ya Siku hiyo ya Sheria Zanzibar, alisema kuwa kuwepo kwa Sheria Namba 14 ya mwaka 2015 ambayo ilianza kutumika kwa Tanzania Bara tarehe 1, Septemba 2015 imesaidia kupunguza matumizi mabaya ya mitandao kwa upande wa Tanzania Bara, ambapo baadhi ya wahusika wamekamatwa na kufunguliwa kesi mahkamani. Vile vile baadhi ya vituo hasa vile vilivyokuwa vinajihusisha na matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa njia ya mitandao vilifungwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wake imeweka masharti makali kwenye baadhi ya Sheria za



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na Jaji Mkuu wa Zanzibar Omar Othman Makungu na Jiji Mkuu Tanzania Mohammmed Chande Othman wakati alipowasili viwanja vya Victoria Garden katika kilele cha sherehe za Siku ya Sheria Zanzibar tarehe 10 Februari, 2016*

Zanzibar zinazohusiana na masuala ya mitandao pamoja na adhabu kwa wale wote ambao wataitumia vibaya mitandao.

Miongoni mwa Sheria hizo ni Sheria ya Baraza la Sanaa Namba 7 ya mwaka 2015 ambayo imekataza matumizi mabaya ya mitandao. Pamoja na mambo mengine, Sheria hiyo imeweka masharti na indhari katika wajibu wa watoa huduma za mitandao kuchukua tahadhari wakati wa kutoa huduma hizo.

Kwa kutambua kuwa matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ni chanzo cha uvunjifu wa Sheria na amani ya nchi, ni vyema Sheria ya Makosa ya Mitandao iliyoanza kutumika nchini Septemba mosi mwaka 2015 kwa upande wa Tanzania Bara baada ya kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusainiwa na Rais Jakaya Kikwete, ikaharakishwa kuridhiwa kutumika Zanzibar, hasa kwa vile Sheria hiyo ililengwa pia kutumika Zanzibar, kwani matumizi mabaya ya mitandao hapa Zanzibar yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku.

Sheria hiyo inaeleza wazi kwamba, wavunjaji wa Sheria hiyo wanaweza kukabiliwa na vifungo vya gerezani au faini ya fedha isiyopungua Sh. milioni tano kulingana na kosa lililofanyika. Kutokana na ukweli kuwa Sheria yenyewe ilishapitishwa na wabunge, ni vizuri sasa Watanzania wakazingatia utekelezaji wake ili kujiepusha na adhabu zake. Aidha, Sheria hiyo imeweka utaratibu wa kulinda na kushughulikia changamoto ya matumizi mabaya ya mitandao ili isiwe chanzo cha uvunjifu wa Sheria na amani ya nchi.



Kamisheni ya Utalii Zanzibar imetoa taarifa ya hali ya kuingiaji watalii Zanzibar kwa mwaka 2015 ambapo kwa mujibu wa taarifa hiyo, Idadi ya wageni walioingia moja kwa moja kutoka nchi zao imeongezeka kinyume na watalii wanaoingia kupitia nchi nyengine za Afrika. Ifuatayo ni taarifa ya kamisheni hiyo kama ilivyotolewa kwenye Jarida la Ikulu.

**1. UTANGULIZI**

Kufuatia juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa sekta ya utalii za kutangaza ndani na nje ya nchi vivutio vya Utalii vilivyopo Zanzibar, idadi ya wageni wanaotembelea Zanzibar imeendelea kukua kwa takriban asilimia sita kwa mwaka katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za

# Hali ya uingiaji wa watalii Zanzibar mwaka 2015 imezidi kuimarika

## ■ Zanzibar inajivunia zaidi watalii wanaoingia kutoka nchi za mbali





Watalii mbali mbali wakiingia nchini kwa njia ya Anga

watalii, kazi ambayo inafanywa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Kamisheni ya Utalii na Idara ya Uhamiaji. Kuimarika kwa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za wageni/watalii kumewezesha Zanzibar kupata idadi halisi ya watalii, ambapo mwaka 2014 jumla ya watalii 311,891 walipata nafasi ya kutembelea Zanzibar.

**2. HALI YA UINGIAJI WA WAGENI MWAKA 2015.**

Takwimu zinaonesha kuwa uingiaji wa wageni Zanzibar kwa mwaka 2015 ulikuwa wa kuridhisha ambapo jumla ya wageni wa kimataifa 294,243 walitembelea Zanzibar. Hata hivyo, idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na ile ya mwaka 2014 ambapo idadi ya wageni waliotembelea Zanzibar kipindi cha mwezi wa Januari – Disemba ilifikia 311,891 kama inavyoonekana katika chati nambari 1.

**Chati nambari 1: Idadi ya watalii walioingia Zanzibar mwaka 2010 – 2015**




**Chanzo: Kamisheni ya Utalii, 2016**


Kimsingi takiwmu za watalii wa kimataifa wanaotembelea Zanzibar zimegawika katika makundi mawilli ambayo ni (i) watalii wanaoingia Zanzibar moja kwa moja kutoka katika nchi zao za makazi na (ii) watalii wa kimataifa wanaoingia Zanzibar kupitia Tanzania bara.

- **Idadi ya watalii wanaoingia moja kwa moja (Direct international tourists)**


Idadi ya wageni walioingia moja kwa moja imeongezeka kutoka 212,447 kwa kipindi cha mwezi wa Januari - Disemba mwaka 2014 hadi kufikia 227,205 kwa kipindi kama hicho mwaka 2015 ) kama inavyoonekana katika chati namba 2. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko wageni 14,758. Miongoni mwa sababu za ongezeko hilo ni kuimarika kwa huduma za Utalii zinazotolewa kwa wageni, kuongezeka kwa mashirika ya ndege yanayofika Zanzibar na kuimarika kwa shughuli za utangazaji katika masoko ya zamani na masoko chipukizi yakiwemo masoko ya Poland na Israel kama inavyoonekana katika jaduweli nambari 1.

...

**Chati nambari 2: Idadi ya watalii walioingia moja kwa moja 2014 -2015.**




**Jaduweli nambari 1: Mwenendo wa ukuaji wa Masoko Chipukizi (2014/15)**





**Chanzo: Kamisheni ya Utalii, 2016**

- **Wageni wanaoingia Zanzibar kupitia Tanzania Bara**

Idadi ya wageni wanaoingia Zanzibar kupitia Tanzania bara imepungua kutoka 99,444 mwaka 2014 hadi kufikia 67,051 mwaka 2015 sawa na upungufu wa wageni 32,363 kama inavyoonekana kwenye chati nambari 3.

**Chati nambari 3: Idadi ya Watalii waliongia Zanzibar kutoka Tanzania Bara (2015)**




Kianzio: Kamisheni ya utalii 2016









*Matukio mbali mbali katika picha yanayoonesha hali ya watalii wanavyoingia Zanzibar na kupata fursa za kujionea vivutio mbali mbali vinavyopatikana visiwani humu*









Miongoni mwa sababu zilizopelekea kushuka kwa idadi ya watalii wanaotoka Tanzania bara ni:

- Kupungua kwa wageni walioingia Tanzania Bara kutoka 781,758 (Jan/Agosti) mwaka 2014 hadi 684,585 (Jan/Agosti) mwaka 2015
- Kupungua kwa watalii wanaotembelea Afrika - Kwa mujibu wa shirika la Utalii la Dunia (UNWTO) kwa kipindi cha Januari – Juni 2015, idadi ya watalii walioitembelea Afrika kwa kipindi hicho ilipungua kwa asilimia 10 ukilinganisha na ile ya mwaka jana.
- Aidha, ripoti hiyo imebainisha kuwa watalii waliotembelea Ukanda wa Sahara ikiwemo Afrika Mashariki kwa kipindi cha mwezi wa Januari hadi Juni ilipungua kwa asilimia 4.
- Kadhalika, takwimu za awali za Utalii za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Utalii Duniani (UNWTO) zinaonesha kuwa pamoja na ongezeko la idadi ya watalii duniani, idadi ya watalii waliotembelea Afrika mwaka 2015 ilipungua kwa asilimia tatu (3%). Athari za punguzo hilo kwa hakika limeiathiri Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

## 3. MAONI YA WADAU WA NCHI ZA NJE KUHUSU HALI YA KIUSALAMA BAADA YA UCHAGUZI

Kufuatia kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa Zanzibar uliofanyika tarehe 25/11/2015, kumekuwa na tahadhari zinazotolewa kupitia matamko ya kiserikali na vyombo vya habari vya nje kuhusu hali ya usalama wa Zanzibar. Matamko hayo yanalenga kuwashauri raia wa nchi hizo kuchukua tahadhari za kutosha wanapotembelea Zanzibar kwa kipindi hichi.

Miongoni mwa nchi zilizotoa matamko hayo ni pamoja na Uingereza, Canada na Australia. Vilevile baadhi ya Magazeti yakiwemo "The New York Times" na "Washington Post" ya Marekani yamekuwa yakitoa taarifa hasi kuhusu usalama wa Zanzibar jambo ambalo linaathiri maamuzi ya wageni wanaopenda kutembelea Zanzibar.

Aidha kumekuwa na mtizamo mzuri wa mitandao ya kijamii ya kimataifa kama vile "trip advisor" kuhusu hali ya usalama ya Zanzibar wakati na baada ya uchaguzi. Watalii wengi waliopata nafasi ya kutembelea Zanzibar katika kipindi hicho wameweza kutoa ushawishi kwa watu wanaotaka kuitembelea Zanzibar wakiamini kwamba hali ya kisiasa ni tulivu na hakuna matukio yenye kutishia usalama wa wageni.

## 4. HITIMISHO.

Takwimu zinaonesha wazi kuwa uingiaji wa watalii hapa Zanzibar haujaathirika na uchaguzi kinyume na muono wa baadhi ya wawekezaji na wadau wa utalii kwamba hali ya kisiasa Zanzibar hasa kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi na ukimya wa Serikali juu ya siku ya kurejewa kwa uchaguzi huo kumeathiri na kunaendelea kuathiri sekta ya utalii Zanzibar (Angalia kiambatanisho nambari 1). Mwezi pekee ambao tulipata upungufu wa watalii ni Octoba jambo ambalo lilikadiriwa kutokea hapo awali. Hata hivyo, tunazo taarifa kuwa baadhi ya wananchi wamekuwa wakitoa taarifa zenye kupotosha kwa wageni kuhusu hali ya utulivu wa kisiasa Zanzibar. Aidha kwa mwezi wa Januari hali imeendelea kuwa nzuri kwani jumla ya watalii 31,717 wameingia ukilinganisha na wageni 23,052 walioingia kipindi kama hicho kwa mwaka 2015.



# Harakati za ujenzi wa barabara ya Fuoni - Mwanakwerekwe zinavyoendelea kwa kasi

Mandhari ya maeneo yanayopita barabara ya Fuoni kutokea Mwanakwerekwe yameanza kuonekana katika hali tofauti kwa wale waliozowea kupita kwenye barabara hiyo hadi siku chache zilizopita.

Barabara hii hivi sasa inapitika kwa shida kutokana na vumbi, matuta makubwa na mashimo kufuatia kazi kubwa inayofanyika ya bomoa bomoa ya nyumba na maduka yaliyokuwa yamejengwa ndani ya eneo la barabara na vile vile uwekwaji wa kifusi kwenye barabara hiyo.

Utekelezaji wa mradi huu ni hatua nyengine ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukamilisha ahadi zake kwa wananchi kama zilivyoelezwa kwenye Ilani ya CCM 2010 – 2015, ambayo kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Ilani hiyo imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 90.

Aidha, ujenzi wa barabara hii ya Fuoni hadi Mwanakwerekwe ni utekelezaji wa mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuzijenga upya barabara zote zinazoingia mjini kutoka mashamba.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ziliingia mkataba na kampuni ya Mwananchi Engineering Contracting Company (MECCO) ya Dar es Salaam kuifanyia matengenezo barabara ya Mwanakwerekwe Makaburini hadi Fuoni kwa kiwango cha Kifusi yenye urefu wa Km 4 ikiwa na njia mbili zenye upana wa mita 6.5 kila upande.

Ili kurahisisha utumiaji wa barabara hii kwa waendao kwa miguu, kutakuwa na upana wa kutosha katikati ya barabara hii kuwawezesha watumiaji hao wa barabara kusubiri wakati wanapokatisha na huku magari yanapokuwa yakipita. Kwa ujumla wake, barabara hii ina urefu wa kilomita 16.3 ikianzia Tunguu, Fuoni, Magomeni, Kariakoo hadi Mkunazini.

Kazi hii inasimamiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara yake ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB). Mkataba wa ujenzi kati ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ulianza tarehe 18 Septemba 2015 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita (6) tangu kuanza kazi hii.

Mradi huu ulitarajiwa kugharimu kiasi ya shilingi bilioni 3.8 ingawa gharama hizo pamoja na muda uliopangwa vinatarajiwa kuongezeka



*Picha zinazoonesha hatua za ujenzi wa barabara kutoka Mwanakwerekwe hadi Fuoni unavyoendelea kwa kasi*

kutokana na changamoto mbali mbali zilizojitokeza baada ya kuanza kazi za ujenzi ikiwa ni pamoja na kukutikana kina kikubwa cha maji kwenye maeneo ya meli tano.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imelazimika kuchukua hatua ya kuanza kuijenga barabara hiyo kwa kutumia fedha zake za ndani katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, kutokana na msongomano mkubwa wa magari kwenye barabara ya zamani, unaotokana na kuongezeka kwa harakati nyingi za kijamii kwenye maeneo ya njia hiyo, ikiwemo kuanzishwa kwa vyuo vikuu maeneo ya Tunguu na ujenzi wa makaazi mapya ya wananchi katika vijiji vya Fuoni, Jumbi, Tunguu na maeneo mengine kwenye muelekeo wa barabara hiyo.

Kwa mujibu wa Meneja wa mradi huo Bwana Japhet Manambi, mara mradi huu utakapokamilika kwa kiwango cha kifusi, kazi itakayofuatia ni kutathmini na kuanza kazi ya utiaji wa lami barabara hii ili kulinda kazi ya awali ambayo itakuwa imekamilika na kukabidhiwa kwa muda chini ya uangalizi wa mjenzi wa awamu ya kwanza.

Tofauti na ujenzi wa barabara nyingi za Zanzibar, ujenzi wa barabara hii umezingatia kwa kina mahitaji ya miundombinu ya baadae kwa mahitaji ya lazima ya wakaazi wanaoendelea kuhamia maeneo yanayopita barabara hiyo kwa kuweka maeneo ya kupitishia mabomba ya maji na huduma nyengine za aina hiyo bila ya kuvunja barabara.

Ili kuendeleza kazi ya kuimarisha miundombinu ya barabara, katika kipindi cha 2015 – 2020, Serikali inakusudia kuendeleza kazi ya utunzaji na utengenezaji wa barabara zilizokwishakujengwa na kufanya marekebisho katika maeneo mbali mbali yanayotuama maji ya mvua na kuathiri ubora wa barabara hizo.

Kwa jumla katika kipindi hicho, Serikali inakusudia kujenga jumla ya kilomita 160.8 za barabara kwa kiwango cha lami Unguja na kilomita 51.1 za barabara kwa kiwango cha lami huko Pemba.



# Matukio mbali mbali katika Picha



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi Vifaa vya Michezo Nahodha wa Timu ya Mafunzo Mpira wa Miguu Haji Ramadhan Mwambe katika hafla iliyofanyika Ikulu Mjini Unguja, tarehe 29 Januari 2016. Katikati ni Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Zanzibar Bi. Sharifa Khamis*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi wakipiga makofi na kuimba wimbo maalum wakati wa chakula cha mchana alichowaandalia vijana walioshiriki Halaiki ya sherehe za Maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika viwanja vya ukumbi wa Salama Bwawani Mjini Unguja tarehe 6, Februari 2016*



*Askari wa vikosi vya ulinzi walioshiriki sherehe za Maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar wakichukua chakula cha mchana kilichotayarishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika viwanja vya Makao Makuu ya Polisi Ziwani Mjini Unguja, tarehe 07, Februari 2016*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli akisalimiana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika sherehe za uzinduzi wa barabara ya Arusha - Holili, Tengeru Mkoani Arusha tarehe 03 Machi, 2016*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwasalimia wananchi waliohudhuria katika viwanja vya Hoteli ya Ngurdoto Mkoani Arusha palipofanyika mkutano wa 17 wa Nchi za Afrika ya Mashariki EAC, tarehe 03 Machi, 2016*



*Baadhi ya vijana walioshiriki halaiki katika sherehe za Maadhimisho ya miaka 52 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar wakiwa katika hafla ya chakula cha mchana kilichoandaliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika viwanja vya ukumbi wa Salama Bwawani Mjini Unguja tarehe 6, Februari 2016*



# Mafanikio ya Mapinduzi ya Kilimo Zanzibar

- Wakulima wamekiri kuwa kilimo ni bora kuliko kazi ya kuajiriwa

Mapinduzi ni msamiati wa Kiswahili ambao umetafsiriwa kwenye kamusi la Kiswahili fasaha kuwa ni mabadiliko ya kiutawala ya haraka katika jamii yanayolazimishwa na wananchi. Maana nyengine ya msamiati huo ni mabadiliko ya makusudi katika mfumo wa kiuchumi na kiutamaduni.

Lakini historia na mazingira ya kisiasa Zanzibar, yameifanya tafsiri ya neno hilo kubeba maana ya kisiasa zaidi ikinasibishwa na Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, ambapo wananchi wa Zanzibar walilazimisha kufanya mabadiliko ya haraka ya kiutawala kuiondoa madarakani serikali ya kikoloni ambayo ilitawala kwa miaka kadhaa.

Haikuwa bahati mbaya kwa Chama Cha Mapinduzi CCM kutangaza Mapinduzi ya Kilimo ndani ya Ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2010 – 2015, ambayo wagombea wa Chama hicho walipita maeneo mbali mbali kuinadi wakati walipokuwa wakiomba ridhaa ya kuongoza nchi. Hatua hiyo ilimaanisha tafsiri ya pili ya msamiati huu ikilenga mabadiliko ya makusudi katika mfumo wa kiuchumi.

Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa sekta ya kilimo katika kujenga uchumi wa kisasa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM iliahidi kuendelea kuimarisha Mapinduzi ya Kilimo kwa kutekeleza mambo mbali mbali ikiwemo kuendelea kuhimiza na kutilia mkazo mafunzo na matumizi ya kanuni za kilimo bora kwa mazao ya chakula, biashara na matunda, huduma za ugani sambamba na kuendelea kukiimarisha Chuo cha Kilimo cha Kizimbani na kuendeleza utafiti wa mbegu bora za mazao ya chakula, biashara na mboga mboga.



*Bwana Abdallah Moh'd Ali Mkulima wa mazao ya mboga mboga katika shamba la Mtakata Kisiwani Pemba*



*Bwana Shaaban Ameir (Sharji) Mkulima wa mazao ya mboga mboga kijiji cha Bungi Kisiwani Unguja*

Miaka mitano baada ya wananchi kuichagua Serikali ya CCM, wakulima wanayo fahari kubwa ya kujivunia mafanikio wanayoyapata katika sekta ya kilimo baada ya kuondokana na kilimo kilichokuwa kimezoeleka yaani kilimo cha kujikimu "subsistence farming" na kujiingiza kwenye kilimo cha biashara "commercial farming".

Mafanikio ya sekta ya kilimo Zanzibar yanatokana na mabadiliko makubwa yaliyopata kasi zaidi ndani ya kipindi cha miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2015, chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani la USAID. Mabadiliko hayo yamejikita zaidi kwenye matumizi ya mbegu bora na umwagiliaji hasa katika kilimo cha mboga mboga.

Mtaalamu wa masuala ya kilimo cha mboga mboga ambaye amefanyakazi katika Shirika hilo la



Marekani linaloshughulikia misaada USAID Bwana Suleiman Said (China) amesema kupitia kilimo cha kisasa cha umwagiliaji, mkulima anaweza kwa uchache kupata mazao yenye thamani ya kati ya Shilingi milioni 15 – 20 za Tanzania ndani ya msimu mmoja wa kilimo, katika shamba lenye ukubwa wa nusu hadi ekari moja kutegemea na aina ya mazao yanayolimwa kwenye msimu husika. Mazao makubwa yanayolimwa na wakulima wa Unguja na Pemba kwa sasa ni matikiti maji, pilipili boga na tungule.

China amesema maendeleo ya kilimo yamepelekea kubadilisha mfumo wa chakula katika maisha ya kila siku ya wananchi wa Zanzibar, ambao katika siku za hivi karibuni wamekuwa watumiaji wakubwa wa matunda ya aina mbali mbali ikiwemo tikiti maji, tunda ambalo amesema lina virutubisho vingi na hivyo kuimarisha afya za wananchi.

Kutokana na mafanikio yanayoonekana ndani ya sekta ya kilimo, wananchi wengi wa Zanzibar wameamua kujiingiza kwenye kilimo cha biashara ambacho kimeonesha kuwa na tija zaidi kuliko aina nyengine ya biashara. Aidha, kilimo cha biashara kimeonekana kuwa na tija zaidi hata kuliko ajira Serikalini.

Bwana China ameliambia Jarida hili kuwa wafanyabiashara maarufu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakifanya biashara ya uagiziaji na uuzaji wa vifaa vya ujenzi Pemba, wameachana na biashara hizo na kujiingiza kwenye kilimo cha biashara.

Kwa upande wa Pemba wakulima wengi wa mboga mboga wanapatikana katika maeneo ya Pujini na shamba la Serikali la Mtakata liliopo Wawi Wilaya ya Chake chake Pemba linalomilikiwa na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ambalo limetolewa kwa wananchi kuendeleza kilimo cha muda mfupi cha mboga mboga. Kwa upande wa Zanzibar ukiachilia maeneo ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakitumika kwa kilimo hicho cha mboga mboga, ardhi ya maweni hivi sasa nayo imekuwa ikitumika vyema kwa kuendeleza kilimo hicho.

Baadhi ya wafanyakazi wa zamani waliokuwa wakifanyakazi serikalini na kwenye makampuni ya watu binafsi na baadae kustaafu, wamesikika wakijutia uamuzi wao wa awali wa kile walichokisema kuwa kupoteza muda mrefu kwenye ajira zenye tija ndogo ikilinganishwa na kilimo hicho cha biashara.

Bwana Shaaban Ameir (Sharji) mkulima wa kilimo cha nje na kilimo cha ndani (green house farming) cha biashara kwa takriban miaka mitatu sasa, amekaririwa na jarida hili akisema kuwa amepata mafanikio makubwa ya aina yake kwenye kilimo cha biashara na angetamani kuanza kazi hiyo miaka mingi zaidi iliyopita.

Sharji ambaye hakutaka kusema wastani wa fedha anazozipata kutokana na kazi yake hiyo kwa mwezi, amekiri kuwa kilimo cha kisasa ndio kazi pekee ambayo itamuwezesha mkulima kuondokana na umasikini wa kipato.

"Serikalini huwezi kupata utajiri iwapo utafanyakazi kihalali, wenye kufaidika ni wale wenye nafasi ya kupata fedha nje ya mishahara yao au watakaoutumia muda wa kazi kufanya shughuli zao binafsi, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu na kanuni za utumishi wa umma", alisema Sharji.

Bwana Mohamed Nuru na Issa Kamata wa Mtule ambao vile vile wanajishughulisha na kilimo cha biashara cha tungule, pilipili boga na tikiti maji, kwa pamoja wamelithibitishia jarida hili kwamba kilimo hicho kinaweza kuwaingizia wastani wa kati ya shilingi milioni 15 hadi 20 kwa ekari moja ndani ya miezi mitatu. Aidha, wamesema kilimo kina nafasi kubwa katika kutoa ajira kwa vijana nchini. Hata hivyo wamesema zipo baadhi ya changamoto ambazo iwapo zitafanyiwa kazi ipasavyo, Zanzibar haitakuwa na haja ya kuagiza bidhaa za mboga mboga kutoka Tanzania Bara.





Ongezeko kubwa la wakulima kwenye kilimo cha mboga mboga limepelekea kupungua kwa kiasi kikubwa uagiziaji wa bidhaa za matunda na mboga mboga kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar. Takwimu zinaonesha kuwa uagiziaji wa bidhaa za matunda na mboga mboga umepungua kutoka asilimia 80 mwaka 2009 hadi kufikia chini ya asilimia 40 hivi sasa.

Ni dhahiri, mafanikio hayo yanatokana na juhudi za serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kupitia miradi na program za ASSP, TASAF, PADEP, TAPP na TAHA ambao wamesaidia kuwashajiisha na kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kupata maarifa, ujuzi na mitaji ambayo hatimaye imewafanya kuongeza kipato chao. Inakadiriwa kuwa mazao ya wakulima yamefikia wastani wa tani 25 hadi 45 kwa hekta moja kwa msimu wa kilimo na pato la kila mkulima limeongezeka kutoka wastani wa shilingi mil. 3.5 hadi shilingi mil. 5.075 kwa kila msimu wa kilimo.

Wataalamu wa masuala ya maendeleo wamethibitisha kuwa hakuna hatua ya maendeleo ambayo inaweza kwenda peke yake bila ya kukabiliana na changamoto. Wakulima wa Zanzibar nao hawakusalimika na hili. Changamoto ya soko la bidhaa za mboga mboga limejitokeza hasa kwa wakulima wadogo wadogo kisiwani Pemba.



*Kilimo cha mboga sasa kimekuwa ni biashara kubwa hivyo hulimwa kwa wingi sana katika visiwa vya Unguja na Pemba*

Uzalishaji wa mboga mboga kisiwani humo unaonekana kuwa ni mkubwa kuliko mahitaji halisi ya wananchi wa kisiwa cha Pemba na hivyo kusababisha kuweko bei ndogo ya bidhaa hizo kwa wakulima. Changamoto hiyo inawakabili zaidi wakulima wadogo ambao mazao yao hayajafikia wingi wa kuweza kuyasafirisha kutoka Pemba na kuyapeleka Unguja kwenye soko kubwa ikilinganishwa na Pemba.

Wakizungumzia changamoto hiyo, wadau mbali mbali wa kilimo wamesema njia ya kukabiliana na changamoto hiyo ni kuanzisha Jumuiya itakayoweza kununua na kuyahifadhi mazao ya wakulima ili baadae yaweze kusafirishwa kwenye masoko kulingana na mahitaji.

Aidha, wamesema uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya kushindika matunda na mboga mboga unaweza kwa kiasi kikubwa kuwa ufumbuzi wa tatizo hilo, hasa iwapo kasi ya uzalishaji wa matunda na mboga mboga itaendelea kuongezeka visiwani Unguja na Pemba.

# SMZ inavyokabiliana na changamoto ya ufugaji wa samaki



*Bwawa la kufugia samaki la ushirika wa  Kichakaa si Shangi lililoko Kiuyu Wilaya ya Wete Kisiwani Pemba*

Mwenendo wa maisha ya jamii katika nchi za visiwa, kwa njia moja au nyengine hutegemea shughuli za uvuvi ama wa asili ambao wataalamu wamebaini kuwa hauna tija, au wa kisasa ambao ni endelevu unaozingatia uhifadhi wa mazingira ya bahari na kukuza kipato cha wavuvi.

Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine za visiwa, uvuvi ni shughuli muhimu ya kiuchumi miongoni mwa wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa mwambao wa bahari.

Hata hivyo, ni ukweli uliowazi kwamba kutokana na ukosefu wa zana bora za uvuvi na utaalamu katika kuendeleza uvuvi wa kisasa, wavuvi wadogo wadogo katika maeneo mengi ya Zanzibar kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia zana duni ambazo siyo tu husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, lakini jitihada zao bado hazijawawezesha kujikwamua na umasikini wa kipato kutokana na faida ndogo inayotokana na aina ya uvuvi wanaoufanya.

Kutokana na kutambua tatizo hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba imechukua juhudi mbali mbali za kuleta mapinduzi ya uvuvi na mazao ya baharini ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwahamasisha wavuvi juu ya uanzishwaji wa vikundi vya ushirika na matumizi ya maarifa ya kisasa na zana bora za uvuvi na kuwapatia misaada na mikopo ya zana hizo ili uvuvi wao uwe wa kisasa zaidi.

Wananchi katika maeneo mbali mbali wameonesha kuridhishwa na juhudi hizo za Serikali na wengi tayari wamehamasika kuunda vikundi vya ushirika na jumuiya zinazoshughulikia masuala ya uvuvi na hasa ufugaji wa samaki wa maji baridi na maji chumvi, kufuga kaa, chaza, lulu na viumbe wengine wa baharini.

Lakini kama ilivyo kwenye harakati zote za maendeleo, wafugaji wengi wa samaki wa maji chumvi wamekabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vifaranga vya maji chumvi hasa vya samaki aina ya mwatiko, ambao wamethibitishwa na wataalamu kwamba ni aina pekee ya samaki wenye kustahamili maradhi na mabadiliko ya hali ya hewa.

Katika ziara yake ya kutembelea miradi ya maendeleo Kisiwani Pemba, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alielezwa na wafugaji wa samaki wa Pujini na Mwambe juu ya changamoto hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa inazorotesha juhudi za wafugaji hao. Tatizo kama hilo vile vile linawakabili wavuvi Ndagoni, Gando, Makombeni, Chokocho, Chambani na maeneo mengine yote ya wafugaji wa samaki huko Pemba.

Aidha, wafugaji wa samaki wa Unguja katika maeneo ya Jozani, Donge Mchangani, Muwanda, Shakani, Fukuchani na maeneo mengine mengi wanakabiliwa na changamoto hiyo.

Katika jitihada zake za kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hivi karibuni ilitiliana saini mkataba na Shirika la Kimataifa la Kilimo (FAO) kwa ajili kuanzisha mradi wa kuendeleza shughuli za ufugaji wa samaki wa kisasa utakaogharimu kiasi cha fedha za Marekani USD 3,228,103 kwa lengo la kuinua uzalishaji wa samaki kwa wafugaji wa zao hilo hapa nchini.

Mradi huo wa miaka mitatu utaendeshwa kupitia shirika hilo la FAO, ambalo fedha zake zitatolewa na Serikali ya Korea kupitia shirika lake la Korea  Inetrnational Cooperation Agency (KOICA).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Idara ya Mazao ya Baharini Bwana Mohd Soud, utiaji wa saini huo ulifanyika tarehe 15 Februari 2016, ambapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitia saini kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ndugu Soud alisema katika utekelezaji wa mradi huo kutajengwa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki aina ya Mwatiko ambao kwa sasa ndio aina pekee ya samaki wanaofugwa kupitia maji



yanayotokana na mtiririko wa maji ya bahari. Pia kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vifaranga vya kaa na majongoo ya baharini.

Alisema kituo hicho kinatarajiwa kujengwa katika eneo la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) liliopo Beit-el-ras Unguja. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuchukua muda wa miaka mitatu ambapo kila mwaka tathmini itafanyika ili kujua hali ya utekelezaji na iwapo malengo yaliyowekwa yamefikiwa. Aidha, tathmini hiyo itaweza kubaini iwapo kuna changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa mradi huo.

Katika mwaka wa kwanza na wa pili, mradi utaanza na shughuli za ujenzi wa kituo, ununuzi wa vifaa pamoja na kupata uongozi wa kituo ambao utajumuisha Bodi, ukaguzi na tathmini kabla ya kuzinduliwa rasmi.

Katika uendeshaji wa kituo hicho cha kuzalisha vifaranga, Bodi itakuwa na wajumbe mbali mbali wakiwemo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Shirika la Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na KOICA.

Kadhalika, atakuwepo mtaalamu Muelekezi atakayesimamia shughuli za uendeshaji (Meneja) akisaidiwa na wataalam wawili wa kimataifa, mtaalamu wa masuala ya utawala, fedha na manunuzi na Mratibu wa Mradi.

Mwaka wa pili kituo hicho kinatarajiwa kiwe kinafanyakazi baada ya ununuzi wa mbegu za madume za kuzalishia pamoja na kufanya zoezi la uzalishaji kama utakavyotarajiwa

Katika kuona azma hiyo inafanikiwa kutatolewa mafunzo watakayopewa wafugaji wa samaki pamoja na kuwepo utaratibu wa kutafsiri mafunzo hayo kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ili elimu inayotolewa iweze kuwafikia walengwa kama inavyokusudiwa.

Sambamba na matarajio hayo, kutakuwa na utaratibu mzuri wa kuwepo mpango endelevu wa kufanya utafiti juu ya ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza mradi huo ili utakapomalizika serikali iwe na utaratibu mzuri wa kupatikana kwa masoko ya uhakika kwa wafugaji wa samaki ili kuweza kuwaondoshea usumbufu wafugaji wakati wa uzalishaji na kuelekea kuondokana na umasikini.

*Ndugu Ali Issa Ali mfugaji wa samaki wa ushirika wa Kichakaa si Shangi ulioko Kiuyu Wilaya ya Wete Kisiwani Pemba akiwa katika harakati wa kuvuna samaki wanaofugwa katika bwawa la ushirika huo*



# Dk. Shein amekamilisha ahadi yake Tumbatu



*Bandari ya Tumbatu iliyojengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa wananchi wa Kisiwa hicho. Bandari hiyo imezinduliwa rasmi tarehe 30 Disemba, 2015*

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba kwa mara nyengine tena imewathibitishia kwa vitendo wananchi wa Zanzibar dhamira yake ya kweli ya kupunguza na hatimae kuondosha kabisa kero za siku nyingi ambazo zimekuwa zikiwakabili wananchi wa Zanzibar wanaoishi kwenye visiwa vidogo vidogo zinazotokana na ukosefu wa miundombinu imara ya kiuchumi na huduma za jamii.

Mwanzoni Ilikuwa ikionekana kama simulizi au hadithi za kizamani za paukwa pakawa za amini usiamini, na kwa kweli wengi walibeza wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akipita kuomba kura kwa wananchi kabla ya awamu ya kwanza ya uongozi wake mwaka 2010, alipokuwa akipita na kuahidi mambo kadhaa ikiwemo kuimarisha miundombinu ya kiuchumi kama vile maji, umeme na gati katika visiwa vidogo vidogo vya Unguja na Pemba ambavyo kwa muda mrefu vilikosa huduma hizo.

Kisiwa cha Tumbatu ni moja miongoni mwa visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar ambavyo vilikuwa vikisubiri kwa hamu utekelezwaji wa ahadi ya Dk. Shein ya kujengwa kwa gati ndogo kwenye Wilaya yao ndogo, gati ambayo ingewasaidia kuwapunguzia usumbufu wa usafiri wakati wanapokwenda au wanaporudi Mkokotoni kwa ajili ya mahitaji yao mbali mbali ya mjini hapo na vile vile mjini Unguja.

Jumatano ya tarehe 30 Disemba mwaka 2015 ilikuwa ni siku maalum ya kihistoria iliyokuwa imechangamka kwa shamrashamra na furaha ya aina yake ya wananchi wa Tumbatu, ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mwenyewe alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa gati mpya katika kijiji cha Tumbatu na kukamilisha ahadi yake aliyoitoa wakati wa kampeni. Sherehe hiyo ilifananishwa na ile ya Kisiwa Panza na Makoongwe Pemba ambako wananchi wa visiwa hivyo nao walipatiwa huduma ya umeme kama ilivyokuwa imeahidiwa na yeye Mheshimiwa Rais.

Utekelezaji wa mradi huo wa gati Tumbatu umezidi kujenga matumaini miongoni mwa wananchi hao kwamba mradi mwengine wa ujenzi wa gati



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo wakati alipokuwa akiangalia ramani ya Ujenzi wa Bandari ya Tumbatu kutoka kwa Mhandisi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar Mbarouk Hamadi Mbarouk wakati alipofanya ziara maalum ya kutembelea miradi ya maendeleo katika kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja tarehe 30 Disemba, 2015*

huko Mkokotoni nao utatekelezwa kama ilivyokuwa imepangwa na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la usafiri wa baharini kwa wananchi wa Tumbatu ambao ndio pekee wa kwenda na kurudi kisiwani humo. Tatizo la gati katika kisiwa cha Tumbatu limedumu kwa muda mrefu na limekuwa likishindikana kutekelezwa na awamu zilizopita kutokana na Serikali kushindwa kupata fedha za kutosha kuweza kutekeleza mradi huo.

Pamoja na ukweli huo, utekelezaji wa mradi huo ambao umegharimu kiasi ya Shilingi milioni 374 zilizolipwa kutoka katika hazina ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, unatokana na utashi binafsi wa Dk. Shein kutaka kuona visiwa vyote vidogo vidogo vya Zanzibar vinajitosheleza kwa mahitaji yote muhimu na kuwa visiwa vya mfano duniani.

"Natamani sana kijiji hiki cha Tumbatu kiwe na barabara na kiwe kinang'ara kama ilivyo kwenye vijiji vingine vya wenzetu, na kitakuwa hivyo, inshaallah" alisema Dk. Shein alipokuwa kijijini Tumbatu.

Ni dhahiri, mradi huu wa Gati ni mkombozi mkubwa katika kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wa Tumbatu na utarahisisha masuala ya usafiri, ambapo mazao na bidhaa zote za wakulima zitaweza kufikishwa sokoni kwa urahisi zaidi kwa upande mmoja na kwa upande mwengine zile zinazotoka nje ya Tumbatu zitaweza kuwafikia wananchi wa kijiji hicho kwa wepesi zaidi.

Lakini kama kuna jambo la kujivunia zaidi kwenye utekelezaji wa mradi huo, ni kitendo cha kushuhudia kwa kuona kuwa usimamizi na utaalamu uliotumika katika kujenga gati hiyo umetolewa na mafundi wazalendo, ambao walifanya kazi hiyo mwanzo hadi kukamilika kwa mradi chini ya usimamizi wa Shirika la Bandari la Zanzibar. Hatua hiyo inathibitisha kuwa Zanzibar wapo mafundi wenye uwezo mkubwa iwapo watapatiwa nyenzo za kufanyia kazi.

Utekelezwaji wa mradi huo umeenda sambamba na utekelezwaji wa mradi wa maji safi na salama kijijini humo, ambao nao umekamilika. Mradi huo mpya katika kisiwa hicho nao umeleta faraja kubwa miongoni mwa wananchi wa Tumbatu, ambao licha ya ukweli kwamba maji ni uhai, huduma hiyo kwa muda mrefu imekuwa ikileta changamoto kisiwani humo.

Wakati Serikali imejidhatiti kutekeleza miradi hiyo kwa maslahi ya jamii na maendeleo, wananchi kwa upande wao wanabaki na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa miradi hiyo inadumu ili iweze kutumika kwa maslahi ya watu waliopo sasa na vizazi vijavyo.

Akitembelea miradi hiyo, Dk. Shein hakuchelea kuwaahidi wananchi wa Kisiwa hicho kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukua juhudi zote kuhakikisha kuwa miradi hiyo na mengineyo katika kisiwa hicho inafanikiwa na inaleta manufaa kwa

Wanatumbatu na wananchi wengine wanaoishi nje ya visiwa hivyo.

Dk. Shein aliwaahidi wananchi wa Tumbatu kuwa matangi kwa ajili ya maji yatajengwa kisiwani humo na Serikali kwani uwezo huo inayo sambamba na kuendeleza hatua nyengine zote katika kuhakikisha miradi yote ya maendeleo katika kisiwa hicho inatekelezwa.

Kauli hiyo ya Dk. Shein inapingana kabisa na kauli za wapinga maendeleo ambao wamejipa kazi maalum ya kupinga shughuli zote za maendeleo zinazofanywa na serikali huku wao wenyewe wakishindwa kuonesha angalau mfano mmoja wa shughuli waliyoifanya kwa maslahi ya wananchi kwenye maeneo wanayoishi. Dk. Shein aliwataka wananchi wa Tumbatu kuwapuuza wale wote wanaobeza miradi hiyo kwani alisema hulka hizo ni miongoni mwa hulka za baadhi ya wanaadamu. Alisisitiza kuwa mwanaadamu yeyote anayepata neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu hanabudi kuishukuru neema hiyo badala ya kuikufuru.

Jamii haina budi kuwapongeza wananchi wa Tumbatu kwa kushiriki vyema katika ujenzi wa miradi wakiamini kuwa mjenzi wa nchi ni mwananchi mwenyewe. Uamuzi wa wananchi wenyewe kuonesha moyo wa kujitolea katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili zimeizidishia ari serikali kuharakisha ujenzi wa gati hiyo na ni wazi kwamba kwa utaratibu huo Serikali itaendelea kuwaunga mkono katika kuwapelekea miradi mbali mbali ya maendeleo na hivyo kufikia lile lengo la kukifanya kisiwa hicho kuwa cha kisasa.

Wananchi wa Tumbatu pamoja na viongozi wa kijiji hicho kwa nyakati tofauti walielezea kufurahishwa kwao na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein na hasa katika kutekeleza ahadi zilizoahidiwa na Dk. Shein kwa wananchi wakati alipokuwa akiomba kura.

Mzee Haji Ame mkaazi wa Tumbatu Jongowe akizungumza na mwandishi wa Makala hii alieleza kuwa wazee wa Tumbatu wana kila sababu ya kumpongeza Dk. Shein kwa kuwasaidia katika kuendeleza miradi yao ya maendeleo na kuahidi kuendelea kumuunga mkono katika juhudi zake za kuleta maendeleo.

Bi Asha akionesha tabasamu lisilo na mfano naye hakua nyuma kuelezea fursa walizonazo akina mama wa Tumbatu hivi sasa baada ya utekelezwaji wa ahadi za Dk. Shein katika kisiwa hicho, na kumpongeza Dk. Shein kwa juhudi zake za makusudi za kuhakikisha kuwa wananchi wa Tumbatu wanapata huduma bora za maendeleo zikiwemo huduma za afya, maji safi na salama, umeme, elimu ujenzi wa gati na huduma nyenginezo.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na Wananchi na wanafunzi wa madrasa huku wakisoma Qaswida wakati walipokuwa wakimshindikiza katika ziara ya kuangalia maendeleo ya Miradi ya maendeleo ya Kijiji cha Kichangani Wilaya Ndogo Tumbatu ikiwemo Ujenzi wa Bandari na Maji Safi na Salama tarehe 30 Disemba, 2015*

Kwa maelezo ya uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar, ujenzi wa gati ya Tumbatu umekamilika na kwa upande wa gati ya Mkokotoni mchakato wa ujenzi wake unaendelea na kwamba ndani ya mwaka huu hatua kubwa ya ujenzi itafikiwa. Ujenzi wa gati hiyo mpya ya Tumbatu umegharimu Shilingi milioni 374 na ujenzi wa gati ya Mkokotoni unatarajiwa kugharimu zaidi ya Shilingi Bilioni moja.

Kwa mujibu wa maelezo ya uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar gati hiyo ya Tumbatu ni kwa ajili ya vyombo vyote vidogo vidogo vikiwemo vile vya kienyeji ambapo pia, kumejengwa eneo maalum kwa ajili ya mizigo. Gati mpya ya Mkokotoni itatumika kwa boti ndogo zitakazosafiri baina ya Mkokotoni na Tumbatu lakini vile vile boti kubwa zitakazokuwa zinasafiri baina ya Mkokotoni na Tanzania Bara.

Nao uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ulieleza kuwa mradi mpya wa maji safi na salama kisiwani humo unaotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeshaanza kutoa huduma ambapo mchango mkubwa umetolewa na wananchi wa Tumbatu, Mwakilishi wa jimbo hilo pamoja na Washirika wa Maendeleo wakiwemo Ubalozi wa Marekani na Iran.

Mradi huo unatarajiwa kuwa na visima vitatu ambapo tayari hivi sasa kisima kimoja kilichochimbwa huko Donge Kipange kimeshaanza kazi na vyengine vinaendelea. Kukamilika kwa visima hivyo na kuunganishwa kwake kutaondosha kabisa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa mgao kama ilivyo hivi sasa na badala yake huduma hiyo muhimu itapatikana kwa muda wote wa saa 24.

Mradi huo ambao unatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ZAWA, unajumuisha pia kazi za kulaza mabomba baharini na uchimbaji visima ambapo gharama za mradi huo ni Shilingi Bilioni moja na nusu za Tanzania.

# Wananchi wa Makangale, Jozani na dhamira yao ya kuhifadhi maliasili

Misitu ni rasilimali muhimu ambayo kwa bahati mbaya imekuwa ikitoweka kwa kasi kutokana na ongezeko la mahitaji ya rasilimali hiyo sambamba na ongeko la idadi ya watu.

Hali hiyo imekuwa ikipelekea kuweko na changamoto za aina yake kwa Serikali katika jitihada zake za udhibiti na ulinzi wa misitu hasa ile ya hifadhi ya taifa, ikitiliwa maanani kwamba rasilimali hiyo ni miongoni mwa vivutio vikuu vya utalii hapa Zanzibar.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilidhamiria kusimamia ulinzi na udhibiti wa maeneo ya hifadhi ya misitu ya Taifa ya Jozani, Unguja na Ngezi, Pemba pamoja na misitu mingine ya asili kwa mashirikiano na wananchi na wadau mbali mbali kazi ambayo imefanyika kwa mafanikio makubwa.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wananchi imekuwa ikiendeleza utunzaji wa hifadhi ya wanyamapori walio katika hatari ya kutoweka hasa kimapunju, popo wa Pemba na paa nunga na kuwatumia kama vivutio vya utalii.

Changamoto ya kutekeleza kazi ya uhifadhi wa misitu inatokana na ukweli kwamba wananchi wengi hutegemea rasilimali hiyo kwa mahitaji yao mbali mbali ya kila siku, huku wakichukua juhudi ndogo sana ya kupanda misitu.

Kazi kubwa ambayo imekuwa ikifanywa na Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kwa muda mrefu sasa ni kujaribu kubadilisha uelewa wa jamii kuhusiana na suala la misitu; faida na hasara zake pamoja na kuwashajiisha wananchi kuanzisha miradi mbadala itakayowaongezea kipato bila ya uharibifu wa mazingira.

Kwa kiasi kikubwa matunda ya kazi hii sasa yameanza kuonekana kutokana na wananchi wengi kuanzisha miradi ambayo ni rafiki kwa mazingira. Miradi hii ni ile yenye kuwaletea tija kubwa wananchi bila ya kukata kuni, miti, makaa na shughuli zote zinazohusiana na misitu. Mifano ya miradi hiyo ni ile ya ufugaji wa nyuki kwa kutumia njia za kisasa, ufugaji wa samaki wa maji chumvi na maji baridi na kilimo cha mboga mboga kwa kutumia njia za kisasa za umwagiliaji.



*Kima Punju wakiwa juu ya miti katika maisha yao ya kila siku. Wanyama hawa hupatikana katika msitu wa hifadhi wa Jozani Unguja*



*Msitu wa hifadhi wa Jozani Unguja*

Inatia moyo kuona kuwa wananchi katika maeneo mbali mbali ikiwemo Shehia ya Makangale iliyoko Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Wakulima wenye mashamba Jozani, Shehia ya Pete, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja hatimaye wamekubali kushirikiana na Serikali kuilinda, kuihifadhi na kuitetea rasilimali ya misitu katika maeneo yao ambayo ni msitu wa hifadhi ya Taifa wa Makangale na Msitu wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani Ghuba ya Chwaka.

Katika mahojiano maalum na wananchi wa kijiji cha Makangale, wananchi mbali mbali wa Shehia hiyo ambayo kijiji chao walipewa heshma kubwa ya kufanyika serehe za ufungaji wa Mradi wa Hifadhi ya Misitu Asili (HIMA) walisema watahakikisha wanailinda heshima hiyo kwa kuilinda kwa nguvu zao zote rasilimali hiyo kwa manufaa yao, vizazi vya sasa, vijavyo na taifa kwa jumla.

Wamesema wananchi wenyewe wa Makangale hawana sababu ya kuharibu mazingira kwa kukata misitu kwani wamezaliwa wakiiona rasilimali hiyo kukiwa na miti minene lakini kwa bahati mbaya miti hiyo imekuwa ikiharibiwa kwa kukatwa na kupasuliwa mbao, ujenzi wa nyumba na uchomaji wa tanu za makaa na chokaa.

"Makangale ina hewa safi, rutba nzuri na mvua za mara kwa mara mambo ambayo yamekuwa yakiwanufaisha wananchi wa Makangale" alisema mzee huyo.

Hivi karibuni kijiji cha Makangale kilipata heshima ya kufanyika sherehe za ufungaji wa Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Misitu ya Asili (HIMA), ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Sheha wa Shehia ya Makangale Mohamed Juma Ali alisema kuwa shehia yake kupitia kamati yake ya shehia pamoja na baadhi ya wananchi wamekubaliana kuandaa mikakati kadhaa itakayoweza kusaidia kulinda rasilimali zilizokuwepo ndani ya msitu wa Hifadhi wa Makangale ili kuona inaendelea kubakia.

"Tumekaa kamati nzima ya Shehia na baadhi ya wanavijiji wanaoendesha shughuli zao za maisha kwa kutegemea rasilimali ya msitu kulitafakari suala hilo kwa pamoja na ufumbuzi wake tumepeana majukumu likiwemo la kila mmoja wetu awe mlinzi wa mwezake katika kulinda msitu huo" alisema Sheha Mohamed.

Kwa mujibu wa kamati hiyo ya shehia, mafanikio ya utekelezaji wa mipango iliyopangwa yataondosha kabisa tatizo la uharibifu wa mazingira ambao hufanywa na baadhi ya wananchi wachache ambao uchunguzi umebaini kuwa wengi wao ni kutoka nje ya shehia hiyo.

Salum Mkadam Hamad ambae ni mkaazi wa kijiji cha Makangale alisema tatizo lilipo kwa wananchi wengi ni kuwa na elimu ndogo ya kutambua umuhimu wa faida za misitu na uhifadhi wa mazingira kwa jamii na umma na ndiyo maana watu wamekuwa wakiharibu bila ya huruma rasilimali ya misitu.

Kwa upande wa uhifadhi wa misitu na wanyama adimu Jozani, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, imekubaliana na wakulima wenye mashamba Jozani na wadau wengine



*Msitu wa hifadhi wa Ngezi Pemba*

kuhifadhi maliasili na viumbe hai vilivyomo kwenye eneo hilo.

Katika kufanikisha mpango huo, pande hizo zimekubaliana kutenga fungu maalum la fedha ikiwa ni fidia kwa wakulima wa Jozani ambao, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2008, wakulima hao ndio wenye kuathiriwa zaidi na kimapunju, ikilinganishwa na wakulima wengine wote kwenye eneo hilo la Hifadhi ya Taifa ya Jozani Ghuba ya Chwaka. Lakini Serikali pia imekubali kuweka mazingatio maalum kutenga fungu la fedha kutoka katika fedha za kiingilio zinazolipwa na wageni kuwalipa wanavijiji wa vijiji vingine tisa vinavyozunguuka hifadhi hiyo.

Kwa kuwa fedha za fidia zinazogaiwa kwa wakulima ni kidogo kuweza kukidhi mahitaji ya wakulima, na kwa kuwa wataalamu wanaoshughulikia masuala ya kutembeza wageni kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamika kutokana muda mdogo wanaoutumia Jozani kwa wageni wao kuangalia kimapunju, msitu wa asili na daraja la mikoko, Umoja wa Wenye Mashamba Jozani (UWEMAJO) umeamua kubuni mbinu mbadala za kuendesha maisha ya wakulima kwa kuanzisha utalii wa kimazingira badala ya kutegemea mazao ya kilimo ambayo yanaathiriwa na kimapunju.

Mradi wa uhifadhi wa kasa ni mradi wa kwanza kubuniwa na wakulima wa Jozani. Kwa kuwa kasa yumo kwenye orodha ya samaki wanaoendelea kupungua kwa kasi duniani, UWEMAJO imeamua kuanzisha kampeni maalum ya kuwahifadhi samaki hao kwa kuwataka wananchi waache kuwatumia kama kitoweleo au chakula. Kasa wanaohifadhiwa Jozani ni wale ambao ama kwa makusudi au kwa bahati mbaya wameingia kwenye mikono ya wavuvi na wamo katika hatari ya kutaka kuliwa.

Jumuiya inawaokoa kasa hao kutoka katika mikono ya wavuvi na kuwahifadhi kwa muda maalum kabla ya kuwapeleka bahari kuu kuendelea na maisha yao ya kawaida. Mradi huu umekuwa kivutio kikubwa kwa watalii wanaotembelea Zanzibar na hasa wanapofika Jozani.

Ufugaji wa samaki ni mradi mwengine wa pili uliobuniwa na wakulima kwa lengo la kupanua wigo wa miradi, kuongeza kipato chao kwa kuvuna samaki na kuuzwa kwa wananchi na kwenye hoteli za kitalii. Pamoja na kuongeza kipato cha wananchi, mradi huu pia ulilenga kuimarisha afya ya jamii kwa kuipatia chakula bora.

Lakini kutokana na kushindwa kufikia lengo hilo kwa sababu ya ukosefu wa vifaranga, mradi huu nao umejumuika na miradi mingine ya utalii, ambapo wageni wamekuwa wakivutika na kuangalia namna ya ufugaji wa samaki. Kadhalika, mradi huu umekuwa ukitumiwa na wasomi na hasa wanasayansi mbali mbali kufanya utafiti kuhusiana na masuala ya ufugaji wa samaki.

Mradi mwengine uliobuniwa na wenye mashamba Jozani ni mradi wa kuhifadhi makobe. Awali mradi huu ulikuwa na makobe wadogo

wachache wenye asili ya Tanzania Bara, lakini kiu kubwa na ya muda mrefu ya wakulima hawa ilikuwa ni kupata makobe wakubwa wa Zanzibar.

Tarehe 8 Mei 2012, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara ya kutembelea miradi mbali mbali ya maendeleo ya wananchi ikiwemo mradi wa Wenye Mashamba Jozani.

Katika taarifa yao kwa Mheshimiwa Rais, wakulima hao walimuomba Dk. Ali Mohamed Shein kuwapatia makobe walioko katika Kisiwa cha Changuu ili waweze kupanua wigo wa biashara yao. Kwa kuzingatia dhana ya utalii kwa wote, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikubali ombi hilo na kuiamuru taasisi husika kuwapatia makobe wakubwa wakulima hao kutoka kisiwa cha Changuu ambako idadi yao imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa. Makobe hao wameongeza haiba ya eneo hilo na wageni wengi wameonekana kufurahia kivutio hicho.

Miradi mingine ya utalii iliyoanzishwa na wenye mashamba ni kwa ajili ya watalii ni mkahawa unaopika chakula cha asili na aina nyengine ya vyakula, mradi wa kuonesha vitu vya asili ambavyo vilitumika kabla ya maendeleo makubwa ya Sayansi na Teknolojia, mapishi ya asili, ngoma za jadi na ziara ya kuangalia pango la Pangejuu.

Hivyo UWEMAJO imefanikiwa kuigeuza athari ya kimapunju kwenye mashamba ya wakulima na kuwa fursa adhimu kwao kuweza kujikwamua na hali ngumu ya maisha kwa kuimarisha utalii wa kimazingira badala ya kukata kuni, makaa na miti ya kujengea, kazi ambazo siyo tu zinahitaji nguvu kubwa na kutoa kipato kidogo, lakini vile vile zinapelekea uharibifu mkubwa wa mazingira.



